# HOTUBA YA WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO, MHE. NAPE MOSES NNAUYE (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2016/2017

## A. UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo kwenye Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, sasa naomba kutoa hoja ya kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa iliyokuwa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka wa fedha 2015/2016. Naomba pia Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Mpango na Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote nampongeza Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuchaguliwa kwake kuwa Rais wa Awamu ya Tano wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nampongeza pia kwa namna alivyoanza kwa kasi kutekeleza Kauli Mbiu ya **‘Hapa Kazi Tu’**. Aidha, nampongeza Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kuchaguliwa tena kuiongoza Zanzibar katika kipindi kingine cha miaka mitano.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie pia fursa hii kumpongeza Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunampongeza kwa dhati kwa sababu ameandika historia ya kuwa Makamu wa Rais mwanamke wa kwanza katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** nampongeza Mhe. Majaliwa Kassim Majaliwa kwa kuteuliwa na Mhe. Rais kuwa Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, nawapongeza Mawaziri wote walioteuliwa kuongoza Wizara mbalimbali katika Serikali ya Awamu ya Tano. Pia nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote ambao wameaminiwa na kuchaguliwa na wananchi kuwa wawakilishi wao katika Bunge la 11 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee kabisa napenda kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la 11 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na pia Mhe. Dkt. Tulia Ackson Mwansasu kuwa Naibu Spika. Vilevile, nawapongeza Wenyeviti wa Bunge kwa kuchaguliwa kwao ili kusaidia kuliongoza Bunge hili. Ni imani yangu kuwa hekima, umahiri na busara zenu katika kuliongoza Bunge hili Tukufu zitaendelea kutumika ili kutekeleza kauli mbiu ya **Hapa Kazi Tu**.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuwapongeza Wenyeviti na wajumbe wa Kamati mbalimbali za Kudumu za Bunge kwa kuchaguliwa kwao kuendelea kuishauri Serikali kupitia Kamati zao. Pongezi za dhati ziende kwa Mwenyekiti Mhe. Peter Joseph Serukamba (Mb), na Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa michango, ushauri na ushirikiano walionipa katika kipindi hiki kifupi katika maeneo mbalimbali ya Wizara ninayoiongoza. Wizara itaendelea kuzingatia miongozo na ushauri unaotolewa ili kufikia malengo tuliyojiwekea. Ushauri wa Kamati hii ndio umefanikisha maandalizi ya hotuba hii.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** mimi pamoja na Naibu Waziri Mhe. Anastazia James Wambura (Mb), tunamshukuru Mhe. Rais kwa kutuamini na kututeua kuongoza Wizara hii. Kwa kauli moja tunaahidi kuwa hatutamwangusha katika kusimamia kauli mbiu ya Serikali ya Awamu ya Tano.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** ninawashukuru pia wananchi wa Jimbo la Mtama kwa kunichagua kwa kishindo kuwa Mbunge na mwakilishi wao katika Bunge hili. Ninawaahidi ushirikiano na utumishi uliotukuka katika kipindi chote nitakachokuwa mwakilishi wao. Hali kadhalika, naishukuru familia yangu kwa kunitia moyo katika kutekeleza majukumu yangu.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** ninawapongeza viongozi wote waliolitumikia Taifa letu kwa umakini katika Serikali ya Awamu ya Nne na kuweza kukabidhi madaraka kwa Serikali ya Awamu ya Tano kwa amani na utulivu. Viongozi hao wakuu ni pamoja na Rais Mstaafu, Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Makamu wa Rais Mstaafu Dkt. Mohammed Gharib Bilal na Waziri Mkuu Mstaafu Mhe. Mizengo Peter Pinda ambao misingi yao imara waliyoiweka inatoa dira na mwelekeo kwa Serikali ya Awamu ya Tano katika kutekeleza majukumu yake.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa moyo wa dhati nampongeza Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Majaliwa Kassim Majaliwa (Mb), kwa hotuba yake fasaha yenye maelezo ya utekelezaji wa kazi za Serikali kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2015/2016 na mwelekeo kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Aidha, nawapongeza Mawaziri wengine wote waliotangulia kuwasilisha hoja zao hapa Bungeni.

11. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inatambua na kuthamini mchango wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii iliyokuwa inaongozwa na Mheshimiwa Said Mtanda na wale wote walioshirikiana nasi katika kipindi cha mwaka wa fedha 2015/2016 katika kutimiza malengo yetu tunawashukuru kwa michango yao.

**12.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mafanikio ya utekelezaji wa majukumu na malengo ya Wizara yamewezekana kutokana na ushirikiano uliopo miongoni mwa viongozi na watumishi wa Wizara na wadau wa sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Shukrani zangu za pekee ziende kwa **Mheshimiwa Anastazia James Wambura (Mb)**, Naibu Waziri ambaye amekuwa msaada mkubwa kwangu, **Prof. Elisante Ole Gabriel**, Katibu Mkuu na **Bibi Nuru Halfan Mrisho Millao**, Naibu Katibu Mkuu. Aidha, nawashukuru Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi, Wakuu wa Vitengo, Wakuu wa Asasi, Wataalamu na Watumishi wote wa Wizara na Asasi zilizo chini ya Wizara kwa kutekeleza kikamilifu majukumu tuliyokabidhiwa.

## B. DIRA, DHIMA NA MAJUKUMU YA WIZARA

**13.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeundwa mwezi Desemba, 2015 kufuatia Serikali mpya ya Awamu ya Tano kuingia madarakani. Wizara hii inasimamia Sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Aidha, katika kusimamia sekta hizi Wizara imejikita kutekeleza dira, dhima na majukumu yaliyopangwa kwa umakini na umahiri mkubwa.

**14.** ***Mheshimiwa Spika,*** dira ya Wizara ni kuwa na Taifa linalohabarishwa vizuri, lililoshamirika kiutamaduni, lenye kazi bora za Sanaa na lenye umahiri mkubwa katika michezo ifikapo mwaka 2025.

**15.** ***Mheshimiwa Spika,*** dhima ni kuendeleza utambulisho wa Taifa kwa kuwezesha upatikanaji stahiki wa habari, kukuza utamaduni, sanaa na michezo kwa lengo la kuleta maendeleo ya jamii kiuchumi.

***16.*** Mheshimiwa Spika, majukumu ya Wizara ni pamoja na kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera za Sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; kuwa Msemaji Mkuu wa Serikali na kusimamia vyombo vya habari nchini; kuratibu na kusimamia maendeleo ya utamaduni nchini; kuratibu na kusimamia maendeleo ya sanaa; kuratibu na kusimamia maendeleo ya michezo nchini; kuendeleza, kuwezesha na kuratibu masuala ya kuwajengea uwezo watumishi wa Wizara; na kusimamia utendaji kazi wa asasi zilizo chini yake (Shirika la Utangazaji Tanzania - TBC, Kampuni ya Magazeti ya Serikali - TSN, Baraza la Sanaa la Taifa - BASATA, Baraza la Kiswahili la Taifa – BAKITA, Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo - TaSUBa, Baraza la Michezo la Taifa - BMT, Bodi ya Filamu na Michezo ya Kuigiza pamoja na Kamati ya Maudhui), miradi na programu zilizo chini ya Wizara.

## C. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA KIPINDI CHA MWAKA 2015/2016

### Mapato

**17.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara ilipanga kukusanya mapato ya jumla ya Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tatu Thelathini na Elfu Nane (**Sh.1,330,008,000**) kutoka vyanzo vyake mbalimbali vya mapato. Hadi kufikia mwezi Machi, 2016 jumla ya Shilingi Bilioni Moja, Milioni Sitini na Saba, Mia Sita na Nne Elfu, Mia Nne na Tisa (**Sh.1,067,604,409**) zilikusanywa ambazo ni sawa na asilimia themanini (80%) ya lengo la makusanyo kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Mchanganuo wa makusanyo upo kwenye ***Kiambatisho Na. I.***

### Matumizi ya Kawaida

**18.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara ilitengewa Shilingi Bilioni Ishirini na Moja, Milioni Mia Tisa Hamsini na Saba, Mia Moja Arobaini na Nane Elfu (**Sh.21,957,148,000**) ikiwa ni Matumizi ya Kawaida ambayo yanajumuisha Mishahara ya Wizara Shilingi Bilioni Nne, Milioni Thelathini na Nne, Mia Tatu Arobaini Elfu (**Sh.4,034,340,000**); Mishahara ya Asasi Shilingi Bilioni Kumi na Mbili, Milioni Mia Nane Themanini na Tatu, Mia Moja Thelathini na Tisa Elfu (**Sh.12,883,139,000**); Matumizi Mengineyo

ya Wizara Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Nne Sitini na Tano, Mia Sita Sitini na Tisa Elfu (**Sh.3,465,669,000**) na Matumizi Mengineyo ya Asasi Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tano Sabini na Nne (**Sh.1,574,000,000**).

**19.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi mwezi Machi, 2016 Shilingi Bilioni Kumi na Mbili, Milioni Mia Tatu Kumi na Mbili, na Ishirini na Sita Elfu, Mia Saba Thelathini na Tisa (**Sh.12,312,026,739**) za Matumizi ya Kawaida zilipokelewa ambazo ni sawa na asilimia 56 ya bajeti ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo Matumizi Mengineyo ni Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Tano Kumi na Tisa, na Sitini na Nne Elfu, Mia Mbili Themanini na Tano (**Sh.2,519,064,285**) na Shilingi Bilioni Tisa, Milioni Mia Saba Tisini na Mbili, Mia Tisa Sitini na Mbili Elfu, Mia Nne Hamsini na Nne (**Sh.9,792,962,454**) ni Mishahara.

**Miradi ya Maendeleo**

**20.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa fedha za maendeleo, mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara ilitengewa Shilingi Bilioni Tatu (**Sh.3,000,000,000**) kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2016 Wizara imepokea Shilingi Bilioni Moja (**Sh.1,000,000,000**) kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

### Utekelezaji wa Majukumu Kisekta

### Sekta ya Habari

***21.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa Fedha 2015/2016, Wizara imeendelea kusimamia Sekta ya Habari na Utangazaji kikamilifu ili kuhakikisha kwamba vyombo vya habari vinatekeleza majukumu yake kwa umakini na kwa kuzingatia weledi. Katika kutekeleza jukumu hilo, Wizara imeendelea kuratibu ushiriki wa Vyombo vya Habari katika matukio mbalimbali ya Kiserikali. Aidha, Wizara imeendelea kuweka mazingira mazuri kwa sekta ya habari kukua na kufanya shughuli zake kwa uhuru zaidi. Mahusiano kati ya Serikali na Asasi zake na Vyombo vya Habari nchini yameendelea kuimarika.

***22.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu programu ya kujenga uwezo wa Vitengo vya Mawasiliano Serikalini katika Wizara, Mikoa, Serikali za Mitaa, Wakala wa Serikali na Taasisi nyingine za Umma kwa kuandaa mafunzo ya kuimarisha Vitengo hivyo ili viweze kusemea na kutoa ufafanuzi kwa weledi na umahiri katika masuala yanayohusu Taasisi zao. Kwa mwaka 2015/2016 mkutano wa Maafisa Habari ulifanyika Morogoro mwezi Machi, 2016 na ulihudhuriwa na Maafisa Habari 202. Katika mkutano huo Maafisa Habari walipata nafasi ya kubadilishana uzoefu na kujenga uwezo wa utendaji na uboreshaji wa kazi. Maafisa hao pamoja na

mambo mengine, wameazimia kila Taasisi ya Serikali kuwa na Mkakati wa Mawasiliano kwa Umma utakaotekelezwa na kufanyiwa tathimini.

**23.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeratibu jumla ya mikutano 115 ya Taasisi za umma na Waandishi wa Habari kwa lengo la kutangaza shughuli za Serikali kwa umma. Vilevile, vipindi 75 vya Taasisi za Umma vimeratibiwa na Wizara na kurushwa kupitia Televisheni ya Taifa na redio ya $\text{TBC}_{\text{Taifa}}$ katika vipindi vya “Jambo Tanzania” na “Tuambie”.

**24.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuwa Msemaji Mkuu wa Serikali kwa kutoa ufafanuzi na maelezo yanayohusu masuala na matukio mbalimbali ya Serikali. Aidha, Wizara ilisimamia kwa ufanisi utendaji wa vyombo vya habari nchini wakati wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 ambapo mchango wa sekta hii ulisaidia kufanyika kwa uchaguzi huo kwa amani na utulivu. Wizara ilichapisha nakala 40,000 za picha ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Hadi Machi, 2016, jumla ya nakala 22,000 zimeuzwa. Hali kadhalika, Wizara imechapisha Bango lenye picha za Baraza la Mawaziri na Kitabu chenye Wasifu wa Wajumbe wa Baraza la Mawaziri wa Serikali ya Awamu ya Tano.

**25.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeratibu utoaji wa ufafanuzi kuhusu hoja na kero mbalimbali za wananchi kwa serikali zilizowasilishwa kupitia Tovuti ya Wananchi. Katika kipindi cha mwezi Julai, 2015 hadi Machi, 2016 jumla ya hoja 93 zilipokelewa. Kati ya hizo, hoja 70 zimepatiwa ufafanuzi na hoja 23 zimeendelea kufanyiwa kazi.

**26.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendeleza uhuru wa Vyombo vya Habari kati ya Julai, 2015 na Machi, 2016 jumla ya magazeti na majarida 18 yamesajiliwa ambapo matatu (3) ni ya Serikali na 15 ya watu binafsi na kufanya jumla ya magazeti na majarida yaliyosajiliwa kuwa 867. Aidha, Vitambulisho 301 vya Waandishi wa Habari (Press Cards) vimetolewa kwa Waandishi wa Habari wenye sifa.

**27.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) ni chombo cha umma chenye wajibu wa kuelimisha, kuburudisha na kuwahabarisha wananchi kuhusiana na masuala mbalimbali yakiwemo ya kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni yanayotokea ndani na nje ya nchi. Licha ya kuwepo changamoto mbalimbali, Shirika hili limeendelea kutekeleza wajibu huo kupitia vyombo vyake vya Redio na Televisheni huku likiendelea kutatua baadhi ya changamoto hizo. Katika kipindi cha mwezi Julai, 2015 hadi Machi, 2016, Shirika limefanikiwa kununua na kufunga mitambo ya kurusha matangazo

ya Redio katika eneo la Kisarawe Mkoa wa Pwani na hivyo kuongeza usikivu katika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani.

***28.*** ***Mheshimiwa Spika,*** mwaka 2015 ulikuwa ni mwaka wa Uchaguzi Mkuu, hivyo, TBC iliandaa vipindi vya kuelimisha jamii kuhusu uchaguzi huo. Aidha, TBC ilirusha matangazo ya moja kwa moja ya sherehe za kuwaapisha Viongozi Wakuu wa Serikali waliochaguliwa, sherehe za kuwaapisha Waheshimiwa Wabunge na uzinduzi wa Bunge la 11.

***29.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/2016 Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) imeendelea kutimiza jukumu lake kuu la kuhabarisha, kuelimisha na kuburidisha jamii kupitia magazeti yake ya Daily News, Sunday News, HabariLeo na SpotiLeo na pia majarida mbalimbali yanayolenga makundi maalum ya wasomaji. Jukumu hili limetekelezwa kwa kutumia weledi wa hali ya juu na kwa kuweka maslahi mapana ya Taifa mbele.

***30.*** ***Mheshimiwa Spika,*** TSN katika mwaka 2015/2016 imeanzisha utaratibu wa kuwaalika wataalam wa fani mbalimbali kuandika makala za kuelimisha jamii ikiwa ni juhudi za kuboresha maudhui ya magazeti yake.

***31.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za kufanikisha Uchaguzi Mkuu, TSN ilitoa

machapisho maalum ya kuhamasisha umma kushiriki katika mchakato wa uchaguzi huo kama sehemu ya majukumu yake ya kuhabarisha, kuelimisha na kuburudisha jamii.

**32.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kampuni ya Magazeti ya Serikali imekamilisha majadiliano ya awali na Benki ya Uwekezaji Tanzania (TIB) ambapo kimsingi imeridhia kutoa mkopo wa asilimia 80 ya gharama za mradi wa upanuzi wa kiwanda cha uchapaji unaotarajiwa kugharimu fedha za Kitanzania bilioni 2.9. Fedha hizo zitatumika kununua mtambo wa uchapaji, kukarabati eneo la kufunga mtambo, kununua malighafi za kuanzia kazi na kulipa wafanyakazi wapya watakao ajiriwa. Kiwanda hicho kitatumika katika kufanya kazi mbalimbali kama vile kuchapa vitabu, kalenda, shajara, majalada na kadi za aina mbalimbali. Tayari Kampuni imeshaweka Shilingi Milioni Mia Tano na Themanini (Sh.580,000,000) kwenye Benki ya Tanzania Investment Bank (TIB) ili kukidhi masharti ya mkopo huo.

**33.** ***Mheshimiwa Spika,*** TSN imeendelea kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa "Central Business Park" utakaojengwa katika kiwanja kilichopo Kitalu Na. 27, Dodoma. Mradi huu unafanyika kwa ubia kati ya TSN na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA). Michoro kwa ajili ya mradi huo imekamilika na imekabidhiwa kwa

mshauri mwelekezi.

34. ***Mheshimiwa Spika,*** Kampuni ya Magazeti ya Serikali imeanza mazungumzo kati yake na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO), Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China na Serikali ya India yenye lengo la kupata fedha za kuboresha Maktaba yake. Aidha, Kampuni imekamilisha zoezi la kuhamisha kumbukumbu na picha kutoka katika mfumo wa analojia kwenda mfumo wa dijiti.

35. ***Mheshimiwa Spika,*** TSN katika mwaka 2015/2016 imewezesha watumishi 15 kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu katika ngazi mbalimbali za elimu. Vilevile, imeendesha mafunzo ya muda mfupi kwa Menejimenti na watumishi wengine katika maeneo mbalimbali kama vile elimu ya kuzuia na kupambana na rushwa pamoja na uandishi wa habari za uchaguzi.

36. ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) inawajibika pia katika Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo katika eneo la Maudhui na Usajili wa Vyombo vya Habari na Utangazaji.

37. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imesajili jumla ya vituo vipya tisa (9) vya Redio na

kufanya idadi ya vituo kufikia 125. Aidha, TCRA imeendelea kusimamia vituo 26 vya Televisheni vinavyofanya kazi hivi sasa. Vituo 15 vya Televisheni vipo katika hatua za ujenzi baada ya kupewa kibali kutoka Wizara yenye dhamana na Habari.

***38.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha Uchaguzi Mkuu unakuwa wa amani, utulivu na wa kuzingatia usawa, TCRA iliandaa kanuni ndogo za uchaguzi za mwaka 2015 ambazo zilitoa mwongozo wa matangazo wakati wa kampeni na uchaguzi mkuu. TCRA pia iliandaa mafunzo kwa watendaji wa vituo vya redio na televisheni juu ya kanuni za utangazaji. Jumla ya watendaji 187 walipata mafunzo ambayo yalitolewa katika Kanda Nne za TCRA.

***39.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia Sekta ya Utangazaji nchini kupitia Kamati ya Maudhui inayoratibiwa na TCRA. Katika kufuatilia kwa karibu maudhui ya vituo vya utangazaji vya Redio na Televisheni, Kamati ilibaini ukiukwaji wa Kanuni za utangazaji katika baadhi ya vituo na ilifanya uamuzi wa kutoa adhabu ya onyo kali na faini kwa vituo vya Channel Ten, Clouds Entertaiment FM, Kahama FM Stereo Redio, Star Television, Tanzania Broadcasting Corporation ($TBC_1$) na Independent Television (ITV).

40. ***Mheshimiwa Spika,*** Kamati ya Maudhui ilitembelea Vituo vya Utangazaji vya mikoa ya Mtwara na Iringa. Katika ziara hiyo, Kamati ilibaini kuwepo vituo visivyokidhi kanuni hasa katika mikataba ya ajira kati ya wamiliki na watumishi. Kamati ilitoa taarifa kwa mamlaka husika kufuatilia mikataba hiyo. Aidha, TCRA inaendelea kuhakikisha kuwa utaratibu wa kuwasilisha wasifu wa wafanyakazi watakaoajiriwa na vituo vinavyoomba leseni unazingatiwa.

**Sekta ya Maendeleo ya Utamaduni**

41. ***Mheshimiwa Spika,*** utamaduni ni chombo cha maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii. Hivyo, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea kusisitiza na kuhamasisha jamii kutambua, kufufua, kukuza, kuhifadhi na kuenzi urithi wa Utamaduni kwa kujiletea maendeleo yao wenyewe na Taifa kwa jumla. Aidha, Wizara imeelimisha jamii kuwa utajiri wa uanuai wa kiutamaduni tulionao ni tunu na utambulisho wa jamii yetu na nyenzo ya kuleta maendeleo endelevu.

42. ***Mheshimiwa Spika,*** Taifa letu linajivunia utamaduni wake ambao una tunu, vitu, mambo au tabia zilizoliwezesha taifa kuwa na utambulisho kwa kujenga umoja, mshikamano, amani na utulivu. Mambo, vitu au tabia zilizochangia utambulisho huu wa Taifa ni pamoja na Lugha ya Kiswahili,

kuheshimu na kuthamini utu, Wimbo wa Taifa, Bendera ya Taifa, maumbile ya asili kama Mlima Kilimanjaro, Mbuga za Serengeti, Kreta ya Ngorongoro na mnyama Twiga.

**43.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na fursa mbalimbali zilizowekewa misingi na kutekelezwa na Wizara, bado utamaduni wetu unakabiliwa na changamoto mbalimbali kama vile matumizi ya mila na desturi zilizopitwa na wakati, mmomonyoko wa maadili, na kutokutumia lugha aushi na adhimu ya Kiswahili kwa ufasaha na usanifu. Sawia na hilo, changamoto nyingine ni kutozingatiwa kwa utamaduni katika maamuzi na mipango ya maendeleo na kutokutumia uzoefu, stadi na elimu ya jadi/asili katika utekelezaji wa miradi, mipango na shughuli za maendeleo.

**44.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na changamoto hizo zinazoikabili Sekta ya Maendeleo ya Utamaduni, Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kufanya tafiti kuweka kumbukumbu na kusambaza taarifa zaidi ya 20 kupitia mitandao ya kijamii, mihadhara na makongamano ya kiutamaduni. Tafiti hizo zilihusu mila na desturi zilizopitwa na wakati ambazo jamii haistahili kuendelea nazo.

**45.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tanzania imefanikiwa kusaini Mkataba wa Uenyeji wa Kamisheni ya Kiswahili ya Jumuiya ya Afrika Mashariki mwezi Desemba, 2015 ambapo Makao Makuu

yake yako Zanzibar. Fursa hii ni heshima kubwa kwa nchi yetu ya Tanzania. Aidha, Wizara inahamasisha jamii kutumia lugha ya Kiswahili kama bidhaa ili kupata ajira na kipato binafsi, cha jamii na taifa sambamba na kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili.

***46.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara imekusanya na kuhifadhi taarifa mbalimbali za Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika kwa kufanya mahojiano na Wazee (Maktaba hai) walioshiriki katika harakati za ukombozi na kupata ushuhuda wao. Taarifa hizi zinatumika kuelimisha umma kuhusu historia ya ukombozi wa nchi yetu na Bara zima la Afrika. Mikoa iliyoshiriki ni pamoja na Dar es Salaam, Pwani, Dodoma na Morogoro.

***47.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara, kupitia Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) iliandaa na kurusha hewani vipindi 28 vya “Lugha ya Taifa” kupitia redio ya $TBC_{Taifa}$, vipindi 28 vya “Kumepambazuka” kupitia Radio One na vipindi 50 vya “Ulimwengu wa Kiswahili” kupitia televisheni ya $TBC_1$. Vipindi hivi hulenga kuelimisha Umma wa Watanzania juu ya makuzi na maendeleo ya lugha ya Kiswahili, vikiwemo msamiati, sarufi na fasihi yake. Hali kadhalika Baraza lilipitia na kutoa Ithibati ya Lugha kwa Miswada 48 ya vitabu vya taaluma.

**_48. Mheshimiwa Spika,_** katika kujenga mazingira ya matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ili kuwezesha maendeleo ya Kiswahili, BAKITA limeanzisha Mradi wa kuunda Kongoo (kopasi) ya Kiswahili ya Taifa inayotarajiwa kuwa na matini andishi yenye jumla ya maneno milioni mia moja (maneno 100,000,000). Matini andishi yenye jumla ya maneno milioni tatu yamekusanywa na kuingizwa kwenye kompyuta kwa njia ya kuskani tangu mradi ulipoanza mwezi Novemba, 2015.

**_49. Mheshimiwa Spika,_** Baraza pia limeratibu na kutoa huduma za tafsiri na ukalimani kwa Asasi na Mashirika mbalimbali, watu binafsi pamoja na mikutano ya Kimataifa. Hali kadhalika limefuatilia matumizi ya Kiswahili na kubaini makosa mbalimbali yaliyofanywa na Vyombo vya Habari na watumiaji wengine wa Kiswahili na kuyasahihisha kwa kutoa ushauri wa matumizi stahiki. Aidha, Baraza katika kujiimarisha limeendelea kuongeza wigo wa kiutendaji kwa kukamilisha uandaaji wa Kamusi Kuu ya Kiswahili. Baraza pia, limeuza nakala 200 za Kitabu cha "Kiswahili kwa wageni".

**Sekta ya Maendeleo ya Sanaa**

**_50. Mheshimiwa Spika,_** Idara ya Maendeleo ya Sanaa imeanzishwa baada ya Serikali ya Awamu ya Tano kuingia madarakani. Kabla ya

hapo Sekta hii ilikuwa inatekeleza majukumu yake chini ya Idara ya Maendeleo ya Utamaduni. Majukumu ya Idara hii ni pamoja na kuratibu na kusimamia shughuli za ukuzaji wa Sanaa na ubunifu kitaifa na kimataifa.

**51.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2015/2016 Wizara kupitia Sekta ya Maendeleo ya Sanaa imefanikiwa kuweka mazingira wezeshi na kufanikisha wasanii na wadau wa Sekta ya Maendeleo ya Sanaa na ubunifu kushiriki katika Tamasha la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni lililofanyika mwezi Agosti, 2015 nchini Kenya. Aidha, Wizara imeendelea kuwahamasisha na kuwasisitiza wasanii kujisajili na kusajili kazi zao ili kulinda haki na maslahi yao kutokana na ongezeko kubwa la maharamia wa kazi za Sanaa.

**52.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na mazingira wezeshi yaliyowekwa na Serikali, mwaka 2016 wasanii wetu wawili walishinda tuzo za 'African Magic Viewers Choice Awards' – AMVCA 2016 huko Nigeria. Wasanii hao ni Bw. Single Mtambalike (Richie) - filamu ya Kitendawili kipengele cha filamu bora lugha ya asili (Kiswahili) na Bi. Elizabeth Michael (Lulu)-filamu ya Mapenzi ya Mungu kipengele cha filamu bora Afrika Mashariki. Vilevile, muongozaji wa filamu ya 'Dogo Masai' Bw. Timoth Conrad alipata tuzo ya 'California Viewers Choice Awards' huko Marekani. Kwa upande wa muziki, wasanii wanne walipata

tuzo mbalimbali nje ya nchi. Jumla ya tuzo 20 zimepatikana kutoka kwa wasanii wafuatao; Bw. Nassib Abdul (Diamond) (17), Bi. Vanessa Mdee (1), Bw. Malimi Mayunga (1) na Bw. Omary Nyembo (Ommy Dimpoz) (1).

***53.*** Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa sanaa ilifanikisha wasanii nchini kupata tuzo za Sanaa kwa mwaka 2015/2016. Tuzo zilizotolewa ni "Tanzania Kilimanjaro Music Awards" 34, "Tuzo za Siku ya Msanii" 4 na "Tuzo za Watu" 13.

***54.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2015/2016 Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) lilisajili jumla ya Wasanii na Wadau wa Sanaa 404 katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Kilimanjaro, Mbeya, Mwanza, Dodoma, Morogoro, Tabora, Iringa, Ruvuma na Tanga. Vilevile, jumla ya kumbi za burudani 53 zilisajiliwa katika Mikoa hiyo.

***55.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza liliendesha mafunzo ya siku tano ya ngoma za asili kwa wanafunzi 80 na walimu 20 wa shule za msingi katika Wilaya ya Masasi Mkoani Mtwara. Aidha, tovuti ya Baraza (www.basata.go.tz) imeboreshwa na kupakiwa taarifa na matukio mbalimbali ya sanaa.

***56.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2015/2016 Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa)

iliendesha mafunzo ya Sanaa ya Stashahada kwa wanachuo 200 na mafunzo ya muda mfupi kwa washiriki 250. Vilevile, ilisimamia na kuendesha Tamasha la 34 la Sanaa na Utamaduni wa Mtanzania, ambalo lilifanyika kwa ufanisi na jumla ya vikundi 52 vya wasanii kutoka ndani ya nchi na vikundi 3 kutoka Kenya, Zimbabwe na Afrika Kusini vilishiriki.

**57.** ***Mheshimiwa Spika,*** TaSUBa imeendelea kutoa elimu ya utamaduni na sanaa kwa kiwango cha astashahada na stashahada. Taasisi, hadi kufikia Machi, 2016, imekamilisha masharti ya NACTE juu ya mtaala wa shahada na kuyawasilisha kwa hatua zinazofuata.

**58.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka wa Fedha 2015/2016 Bodi ya Filamu imepitia jumla ya miswada 165 ambayo ilipewa vibali vya kutengenezea filamu. Aidha, hadi mwezi Machi, 2016 jumla ya "DVD" 658 za filamu zimekaguliwa, kupangiwa madaraja na kupewa vibali sawa na asilimia 91.6 ya lengo la kukagua filamu. Kati ya hizo, filamu 582 ni za ndani ya nchi na filamu 76 zilitoka nje ya nchi. Filamu 1 ilikataliwa na filamu 5 zilielekezwa kufanyiwa marekebisho. Vilevile, elimu ya filamu na sheria zinazosimamia filamu zimeendelea kutolewa kupitia vyombo vya habari, mitandao ya kijamii, vikao vya wadau na maadhimisho mbalimbali ambapo jumla ya wadau 2,455 walifikiwa na jumla ya machapisho 14,100 yalisambazwa.

59. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi imeshiriki katika Mpango wa Kliniki ya Filamu kwa kutoa mada na vyeti kwa washiriki 306. Mpango huo ulilenga kuibua vipaji, kuendesha mafunzo ya uongozaji wa filamu, uandishi wa miswada ya filamu, uboreshaji wa viwango, biashara na utafutaji wa masoko kwa wasanii wa filamu. Kliniki hiyo iliendeshwa kwa kushirikiana na "Swahili Cooperative Society" ya Mkoani Morogoro. Vilevile, Bodi imeendelea kushirikiana na Bodi za filamu za Mikoa na Wilaya ambapo Bodi za Wilaya za Kalambo, Sumbawanga, Meru, Ngara, Misenyi, Urambo, Itilima, Kakonko, Serengeti, Kyerwa, Jiji la Arusha, Manispaa ya Sumbawanga, Lindi, Musoma, Uvinza, Biharamulo na Temeke zimewasilisha taarifa mbalimbali za sekta ya filamu.

60. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi ya Filamu kwa kushirikiana na COSOTA, BASATA na TRA imeshiriki katika urasimishaji wa Tasnia za Filamu na Muziki kwa kuhakikisha kuwa kazi zote za filamu zinazoingia sokoni bila kufuata taratibu zinaondolewa kupitia operesheni. Kwa mwaka wa fedha 2015/2016, jumla ya nakala za filamu 656,579 zenye thamani inayokadiriwa kuwa Shilingi, Bilioni Moja, Milioni Mia Tatu Kumi na Tatu, Mia Moja Hamsini na Nane Elfu (**Sh.1,313,158,000**) zilizoingizwa sokoni bila kufuata taratibu ziliondolewa. Kati ya hizo, kazi 650,101 zinatoka nje ya nchi huku kazi 6,478 zikitoka hapa nchini. Aidha, Bodi ya

Filamu ilisuluhisha migogoro baina ya wadau wa filamu ambapo migogoro mitatu ilipatiwa ufumbuzi.

**Sekta ya Maendeleo ya Michezo**

***61.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Michezo inayo nafasi kubwa katika kuchangia maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika Taifa na miongoni mwa Mataifa. Aidha, michezo ni nyenzo muhimu katika kuimarisha afya, kuhamasisha amani miongoni mwa jamii na kurejesha matumaini kwa watu au jamii iliyofikiwa na maafa.

***62.*** ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Januari 2016, Tanzania iliingia katika historia ya soka barani Afrika baada ya mchezaji wetu Mbwana Ally Samatta kutangazwa kuwa mchezaji bora wa mwaka wa Afrika kwa wachezaji wanaocheza ligi za ndani za Afrika. Aidha, mchezaji Francis Cheka alifanikiwa kuchukuwa mkanda wa Mabara wa uzito wa Super Middle mwezi Februari, 2016. Nachukua fursa hii kuwapongeza kwa dhati vijana wetu hawa na vijana wengine katika Tasnia ya Michezo kwa kulitangaza vyema na kuliletea Taifa letu sifa kubwa. Ninatoa wito kwa vijana wote kuiga mifano hiyo mizuri ya wenzao.

***63.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/2016, Wizara imeendelea kuendesha mafunzo ya Stashahada ya Ufundishaji

Michezo na Utawala wa Michezo katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya. Sambamba na mafunzo ya Stashahada, Chuo pia kilitoa mafunzo ya ufundishaji Michezo kwa Walimu 130 wa shule za Msingi na Sekondari kwa ajili ya maandalizi ya michezo ya UMITASHUMTA na UMISETA. Aidha, jumla ya walimu wa michezo 70 kwa watu wenye ulemavu walihudhuria mafunzo ya muda mfupi katika chuo hicho. Vilevile, mafunzo mengine ya muda mfupi ya ufundishaji, Uongozi na Utawala wa Michezo yalitolewa katika vituo vya michezo vya Songea na Arusha ambapo jumla ya washiriki 224 walinufaika na mafunzo hayo.

**64.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/2016 Wizara iliendelea kuunga mkono jitihada za mashirikisho ya Michezo ya Kimataifa ya kupiga vita matumizi ya dawa na mbinu haramu za kuongeza nguvu kwa wanamichezo. Jumla ya wanamichezo 14 walichukuliwa vipimo vyao na kupelekewa kupimwa katika maabara za Kimataifa na wote kukutwa salama. Aidha, jumla ya maafisa wawili walihudhuria mafunzo ya Kimataifa ya mbinu za upimaji wa wanamichezo dhidi ya matumizi ya dawa hizo.

**65.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Michezo ya Kimataifa, Wizara iligharamia ushiriki wa Timu ya Tanzania katika Michezo ya Afrika (All Africa Games) iliyofanyika huko Kongo Brazzaville mwezi Septemba, 2015. Timu

zilizoshiriki ni za Michezo ya riadha, kuogelea, judo na ngumi. Nyingine ni timu ya kunyanyua vitu vizito kwa watu wenye ulemavu na timu ya mpira wa miguu kwa wanawake.

**66.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2015/2016, Wizara iliendelea na kazi ya Usajili, ambapo hadi mwezi Machi, 2016 jumla ya Vyama vya Michezo sita, Vilabu vya Michezo 116 na Vituo kumi vya Michezo vilikuwa vimesajiliwa. Usajili wa Vyama vya Michezo unafanyika ili kuvipa uhalali vyama hivyo kutambulika na kuendesha shughuli zake kwa mujibu wa sheria za nchi.

**67.** ***Mheshimiswa Spika,*** katika mwaka 2015/2016, Wizara imekamilisha uboreshaji wa Uwanja wa Uhuru kwa kujenga ukuta kuzunguka Uwanja huo. Aidha, Wizara imejenga tanki la maji ili kuhakikisha maji yanapatikana uwanjani hapo wakati wote sambamba na kujenga bomba kubwa la kuondoa maji taka na maji ya mvua katika eneo la uwanja huo. Lengo la maboresho hayo ni kuwezesha wanamichezo, watazamaji na wadau wengine kupata mahali salama pa kufanyia michezo na kupata burudani kwa kadri ya matakwa yao na kwa kuzingatia vigezo na masharti yaliyopo.

**68.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2015/2016 Baraza la Michezo la Taifa liliratibu na kusimamia chaguzi za Vyama vya

Michezo vitatu na Shirikisho moja. Vyama hivyo ni chama cha Mpira wa Mikono Tanzania (TAHA), Chama cha Kuogelea Tanzania (CHAKUTA), Chama cha Michezo ya Vishale (Darts) Tanzania na Shirikisho la Michezo kwa Vyuo vya Elimu ya juu (SHIMIVUTA). Vilevile, mafunzo ya michezo kwa walimu 90 kutoka Wilaya za Mkoa wa Manyara katika Michezo ya soka, riadha, netiboli na mpira wa wavu yametolewa.

**69.** ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza liliendesha mafunzo ya usuluhishi wa migogoro kwa vyama vya Michezo 7 ili kuimarisha ushirikishwaji wa wanachama katika kutatua migogoro yao. Vyama hivyo ni Kamisheni ya Ngumi za Kulipwa, Chama cha Tenisi, Chama cha Michezo ya Jadi Tanzania (CHAMUJATA), Chama cha Michezo ya Kuogelea Tanzania, Chama cha Makocha wa Mchezo wa Kuogelea, Chama cha WUSHU Tanzania na Chama cha Waamuzi wa Mpira wa Miguu Tanzania.

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza limeendelea kuhamasisha jamii kushiriki katika mazoezi ya viungo na michezo ili kujenga misingi imara ya ushiriki kwenye michezo kuanzia umri mdogo kwa lengo la kuibua vipaji vya wanamichezo chipukizi, kujenga afya na kuishi katika michezo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2016 jumla ya vikundi 70 vimeundwa nchi nzima na kushiriki kwenye matamasha ya michezo katika maeneo yao. Pia, Tanzania

ilifanikiwa kuwa mwenyeji wa mashindano ya riadha ya Afrika Mashariki kwa vijana wenye umri chini ya miaka ishirini yaliyoshirikisha nchi kumi na moja ambapo mwanariadha Rose Seif alifanikiwa kupata medali ya dhahabu. Nichukue fursa hii kumpongeza kijana huyo kwa mafanikio na sifa alizoliletea Taifa letu.

**71.** ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza limewapeleka kwenye mafunzo ya muda mrefu watumishi wawili na mtumishi mmoja mafunzo ya muda mfupi kwa lengo la kuboresha utendaji na utekelezaji wa shughuli za Baraza.

**Utawala na Rasilimaliwatu**

**72.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuwawezesha Watumishi kuongeza tija sehemu za kazi. Katika kipindi cha Mwaka 2015/2016 watumishi 17 waliendelea na mafunzo mbalimbali ya muda mrefu na watumishi wapya 30 walihudhuria mafunzo elekezi ya muda mfupi (Induction Course).

**73.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kuzingatia Sera ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma toleo la Mwaka 1999 na 2008 pamoja na taarifa za Upimaji wa Kazi wa Wazi (OPRAS), Wizara imeendelea kusimamia stahili na haki za Watumishi kwa kuwapandisha vyeo Watumishi 24 wenye sifa zinazostahili. Aidha, Watumishi 22 walithibitishwa kazini na wengine wanne walibadilishwa kada baada ya kupata sifa stahiki.

74. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha Utawala Bora kwa kuwashirikisha Watumishi sehemu za kazi kwa kuendesha vikao mbalimbali vya kiutawala ambapo watumishi hupata fursa ya kuchangia katika kuboresha na kuimarisha utendaji kazi.

75. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara imeendeleza juhudi za kupambana na maambukizi ya VVU/UKIMWI mahala pa kazi, kwa kutoa elimu kwa watumishi 100, kuwahamasisha kujitokeza kupima afya zao pamoja na kutoa huduma kwa watumishi wanaoishi na VVU/UKIMWI ambao wamejitokeza.

## D. MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

### Sekta ya Habari

76. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Sekta ya Habari kwa mwaka 2016/2017 inapanga kutekeleza majukumu yafuatayo; kuisemea Serikali katika masuala muhimu yanayohitaji ufafanuzi na kuratibu Vitengo vya Mawasiliano Serikalini; kufuatilia na kutathmini utendaji wa Maafisa Mawasiliano Serikalini katika Wizara, Wakala wa Serikali, Idara za Serikali zinazojitegemea, Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi nyingine za Umma kwa lengo la kuimarisha Vitengo vya Mawasiliano Serikalini; kusimamia na kuboresha shughuli

za vyombo vya habari nchini, ikiwa ni pamoja na kukamilisha mchakato wa utungaji wa Sheria ya Huduma za Habari; na kuwa kiungo muhimu cha mtiririko wa habari nchini kwa kuratibu na kusimamia njia mbalimbali za upashanaji habari ikiwa ni pamoja na kuboresha Tovuti ya Wananchi.

**77.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia itaendelea kusimamia na kuboresha huduma za vyombo vya habari vya serikali, ikiwa ni pamoja na usikivu wa Shirika la Utangazaji la Taifa hasa Mikoa ya pembezoni; kukusanya, kuandika na kusambaza habari mbalimbali za matukio ya Serikali kwa wananchi kupitia vyombo vya habari; kupiga picha za matukio mbalimbali ya Serikali, kuzisambaza katika vyombo vya habari na kuzihifadhi katika makavazi ya Sekta; kuimarisha ukusanyaji wa mapato ikiwa ni pamoja na kusimika mfumo wa kielektroniki wa kuhifadhi na kuuza picha za matukio mbalimbali ya Serikali katika Idara ya Habari Maelezo; kusajili magazeti na machapisho na kuwapatia vitambulisho waandishi wa habari wanaostahili.

**78.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) kwa mwaka 2016/2017 litatekeleza majukumu yafuatayo; kutoa habari za kitaifa na za kimataifa kwa Umma; kuandaa vipindi vya kuelimisha jamii juu ya masuala mbalimbali ya maendeleo, Utamaduni, Sanaa, afya, Uchumi, kilimo na

biashara; kuandaa vipindi mbalimbali vya kuburudisha jamii kupitia michezo, muziki, ngoma za asili na maigizo; na kuongeza upanuzi wa usikivu wa redio katika Mikoa ya pembezoni ya Kigoma (Kasulu na Kakonko), Mara (Tarime), Ruvuma (Nyasa–Mbamba-bay), Tanga (Mkinga-Horohoro), Arusha (Longido-Namanga, Ngorongoro), Kilimanjaro (Rombo) na Lindi (Kilwa -Nangurukuru).

***79.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Kampuni ya Magezeti ya Serikali (TSN) kwa mwaka 2016/2017 itatekeleza majukumu yafuatayo; kusimamia utekelezaji wa mradi wa "Central Business Park" Dodoma unaofanyika kwa ubia kati yake na TCRA; kuendelea na mpango wa mradi wa upanuzi wa kiwanda cha uchapaji; kufanya mafunzo mbalimbali kwa wafanyakazi ili kuongeza tija kwa Kampuni; kuboresha maudhui ya Magazeti ya Serikali; na kutoa machapisho maalum kwa ajili ya kuelimisha jamii kuhusu matuki mbalimbali ya kitaifa. Vilevile, itaendelea kuboresha mfumo wa utunzaji wa taarifa za wafanyakazi kwa kuanzisha mfumo wa dijitali ambao utafanya kazi sambamba na mfumo wa sasa wa mafaili; kupitia na kuboresha Sera mbalimbali za Kampuni pamoja na miongozo ya utumishi kwa wafanyakazi; kuimarisha kitengo cha machapisho kupitia njia ya mtandao; na kutekeleza mradi wa "TSN Education Initiative".

**80.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Kamati ya Maudhui, kwa mwaka 2016/2017 itatekeleza majukumu yafuatayo; kufanya upanuzi wa mtambo wa ufuatiliaji na kufuatilia kwa karibu maudhui ya vituo vyote vya utangazaji; kukamilisha Mwongozo wa Udhamini na Matangazo ya biashara (Code of Advertising and Sponsorships) kwa vituo vya utangazaji nchini; kuratibu mafunzo kwa wakalimani wa lugha ya alama kutoka kwenye vituo vya televisheni ili kuwezesha tafsiri kwa vipindi vya habari na matukio kwa watu wenye ulemavu wa kusikia; na kuendelea kukutana na watendaji na viongozi wa vituo vya utangazaji vya kijamii ili kuboresha maudhui ya vipindi vyao kwa manufaa ya wasilikizaji wa vijijini. Aidha, Mamlaka ya Mawasiliano itaendelea kufanya ukaguzi katika vituo vya utangazaji ili kubaini maafisa ambao hawana sifa za kusimamia na kutangaza katika vituo hivyo ili kuchukua hatua stahiki.

**Sekta ya Maendeleo ya Utamaduni**

**81.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara kupitia sekta ya Maendeleo ya Utamaduni itatekeleza majukumu yafuatayo; Kufuatilia na kutathmini shughuli za Sekta ya Utamaduni ili kubaini fursa na changamoto zilizopo na kuziwekea mipango na mikakati endelevu ya maendeleo ya sekta ikiwemo kutumia utamaduni wetu kiutalii; kuhifadhi na kuziendeleza lugha

za kijamii zilizo katika hatari ya kutoweka au kutozungumzwa kwa minajili ya kulinda utambulisho wake; kuratibu, kufuatilia na kuhimiza shughuli za utafiti na ukuzaji wa fasihi na kukamilisha uhuishaji wa Sera ya Utamaduni na kutunga Sera ya Lugha. Aidha, Wizara itaratibu utafiti, ukusanyaji, uhifadhi na usambazaji wa mila na desturi miongoni mwa jamii zaidi ya 120; kuendesha mjadala wa Kitaifa juu ya maadili ya Mtanzania; kutafiti, kuhifadhi na kukuza lugha za kijamii kwa lengo la kukuza misamiati ya lugha ya Kiswahili na kuanzisha mfumo wa kukusanya taarifa na takwimu za Sekta ya Utamaduni nchini.

**82.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), kwa mwaka 2016/2017 itatekeleza majukumu yafuatayo; kuandaa vipindi 52 vya lugha ya Taifa kupitia redio ya $TBC_{Taifa}$; vipindi 52 vya Kumepambazuka kupitia Radio One na vipindi 52 vya Ulimwengu wa Kiswahili kupitia televisheni ya $TBC_1$; kufanya tafsiri kwa asasi za Serikali, mashirika ya umma na ya binafsi pamoja na watu binafsi; kutoa ithibati ya vitabu vya kiada na ziada; kufanya ukarabati wa jengo la ofisi; na kuandika na kuchapisha vitabu na majarida ya Kiswahili. Aidha, jukumu lingine litakalotekelezwa na BAKITA ni kukusanya matini andishi ya Kiswahili yenye jumla ya maneno milioni kumi na kuyaingiza kwenye kompyuta kwa kuziskani kwa ajili ya Kongoo ya Kiswahili ya Taifa.

### Sekta ya Maendeleo ya Sanaa

**83.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara kupitia Sekta ya Maendeleo ya Sanaa itatekeleza majukumu yafuatayo; kutunga Sera za Maendeleo ya Sanaa na Filamu; kuendesha na kuratibu mpango wa kudumu wa Sanaa kwa wasanii na wadau; kusimamia urasimishaji wa shughuli za Sanaa nchini; kuratibu na kuandaa matamasha ya kitaifa ya sanaa kwa wasanii na wadau nchini; kuratibu na kusimamia uanzishwaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Sanaa nchini; kukusanya na kuhifadhi takwimu za miundombinu ya Sanaa, kazi za Sanaa na wasanii na kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika.

**84.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), kwa mwaka 2016/2017 itatekeleza majukumu yafuatayo; kutoa tuzo za BASATA kwa Wanafunzi tisa wa shule za Sekondari wa masomo ya Sanaa katika fani za muziki, sanaa za maonesho na ufundi (uchoraji); kuandaa na kuratibu Siku ya Msanii ambayo itaenda sambamba na utambuzi na kuthamini mchango wa Wasanii katika Fani za Muziki, Filamu, Sanaa za Ufundi na Maonesho; kuendesha midahalo 32 ya Jukwaa la Sanaa kwa wasanii na wadau wa Sanaa wapatao 3000; kuandaa na Kuratibu

Tuzo za Muziki za Tanzania; kuwajengea uwezo wa kiuongozi viongozi kutoka vyama 30 na Mashirikisho manne (4) ya Wasanii; kukamilisha Ujenzi wa Ukumbi wa Wazi wa Sanaa; na kusogeza huduma za usajili wa kazi za sanaa karibu na wadau yaani Mikoani na Wilayani.

**85.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa), kwa mwaka 2016/2017 itatekeleza majukumu yafuatayo; kutoa mafunzo kwa wanachuo 350; kuendesha Tamasha la 35 la Utamaduni Bagamoyo litakalofanyika Septemba 2016; kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa wafanyakazi na wanachuo hasa upatikanaji wa vitendea kazi, ubora wa masomo, kuboresha miundombinu ya kufundishia, kuboresha mabweni, madarasa na ofisi; kukarabati miundombinu ya Taasisi kwa awamu kutokana na mapato ya ndani; kufuatilia Mtaala wa Shahada NACTE kwa ajili ya kupata Ithibati; kuandaa rasilimaliwatu na miundombinu kwa ajili ya mafunzo ya sanaa na utamaduni kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki; na kuanza ukarabati wa studio ya kisasa ya muziki.

**86.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Filamu, kwa mwaka 2016/2017 itatekeleza majukumu yafuatayo; kurasimisha vibanda 5,000 vya kuonyeshea filamu, kubaini wadau watakaowekeza na kuvipatia leseni; kupitia miswada 199 ya kutengeneza Filamu na kutoa

vibali kwa makampuni ya utengenezaji wa filamu hizo; kukagua na kuwekea madaraja DVD za filamu 1000 na kuzitolea vibali; kuendesha operesheni za kudhibiti filamu zitakazoingia sokoni bila kufuata taratibu; kuratibu, kuandaa na kutoa leseni za uendeshaji na vitambulisho kwa makampuni ya filamu, wadau wanaofanya kazi za filamu na kumbi za sinema; kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Filamu kwa kushirikiana na wadau; na kuimarisha Bodi ya Filamu kwa kununua vitendea kazi na kuajiri watumishi. Aidha, Wizara itaratibu utungaji wa Sera inayohusu shughuli za filamu nchini pamoja na kusogeza huduma za usajili wa kazi za sanaa karibu na wadau yaani mikoani na wilayani.

**Sekta ya Maendeleo ya Michezo**

***87.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara itatekeleza majukumu yafuatayo; kusimamia maendeleo ya michezo nchini; kuboresha mifumo ya usimamizi wa vyama vya michezo nchini ikiwa ni pamoja na kuhuisha Sera ya Michezo na Sheria ya Baraza la Michezo la Taifa Na. 12 ya mwaka 1967 na marekebisho yake Na. 6 ya mwaka 1970; kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali ikiwa ni pamoja na kusimika mfumo wa kielekroniki katika kukusanya mapato yatokanayo na shughuli zinazofanyika katika uwanja wa

Taifa; kuratibu ushiriki wa timu za Taifa katika “Michezo ya Olympic” na “Paralympic” inayotarajiwa kufanyika nchini Brazil mwezi Agosti/Septemba, 2016; kuendelea kudahili wanafunzi na kuendesha mafunzo ya utaalam wa fani mbalimbali za Michezo katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya na Vituo vya Michezo vya Songea na Arusha; kufanya upimaji wa Wachezaji dhidi ya matumizi ya dawa na mbinu haramu za kuongeza nguvu michezoni; kuendelea kutoa huduma ya Kinga na Tiba kwa wanamichezo, wafanyakazi na wadau wengine; kutafuta Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya ugharamiaji wa shughuli mbalimbali za Maendeleo ya Michezo; na kuboresha mifumo ya usimamizi wa Sekta ya Michezo kwa ujumla wake.

**88.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2016/2017 Baraza la Michezo la Taifa litatekeleza majukumu yafuatayo kwa kushirikiana na wadau wengine; kuendeleza mpango wa Michezo kwa jamii kwa kuendesha mafunzo kwa Walimu wa Michezo na utaratibu wa uendeshaji wa Matamasha ya Michezo katika jamii ili kuinua ari na kuongeza hamasa ya ushiriki katika Michezo; kuendelea na maandalizi ya uhuishaji wa Sheria ya Baraza la Michezo la Taifa ili kuendana na mazingira ya sasa kisiasa, kiuchumi na kijamii; kuratibu na kusimamia chaguzi za vyama na mashirikisho ya michezo sita; kuandaa mkakati wa kuongeza ushiriki kwa Wanawake

na watu wenye ulemavu katika Michezo na kugombea nafasi za uongozi katika vyama vya michezo; na kuandaa na kuendesha mafunzo ya Utawala Bora na maandalizi ya mipango mikakati kwa viongozi wa Vyama vya Michezo. Aidha, Tanzania itakuwa mwenyeji wa mashindano ya riadha kwa nchi za Afrika Mashariki kwa vijana wenye umri chini ya miaka 20 katika mwaka 2016/2017.

**Utawala na Rasilimaliwatu**

***89.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2016/2017, Wizara imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo; kuwahimiza Watumishi wanaojitambua kuwa na maambukizi ya VVU/UKIMWI kujitokeza ili kupata msaada pamoja na stahiki nyingine; kuimarisha Utawala Bora kwa kushirikisha Watumishi sehemu za kazi kwa kuendesha vikao mbalimbali vya kiutawala na Baraza la Wafanyakazi; kuhakikisha Wizara inatoa fursa za kujiendeleza kwa Watumishi wenye sifa na ambao wapo katika mpango wa mafunzo wa Wizara; na kuhakikisha Watumishi wote wenye sifa na wanaostahili wanapandishwa vyeo.

## E. MAKADIRIO YA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

### Mapato

***90.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara imepanga kukusanya jumla ya Shilingi Milioni Mia Nane Ishirini na Elfu Tano **(Sh.820,005,000)** kutoka katika vyanzo vyake mbalimbali vya mapato. Mchanganuo wa makusanyo kifungu kwa kifungu upo katika ***Kiambatisho Na. I.***

***91.*** ***Mheshimiwa Spika,*** makusanyo yameshuka kutoka Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tatu Thelathini, na Elfu Nane **(Sh.1,330,008,000)** kwa mwaka wa fedha 2015/2016 hadi Shilingi Milioni Mia Nane Ishirini na Elfu Tano **(Sh.820,005,000)** kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kutokana na makusanyo yaliyokuwa yakikusanywa na Bodi ya Filamu katika Sekta ya Maendeleo ya Utamaduni kuondolewa. Makusanyo hayo yameondolewa baada ya Msajili wa Hazina kuipa Bodi ya Filamu mamlaka kamili ya kuwa Taasisi inayojitegemea kuanzia tarehe 01 Julai, 2016.

### Matumizi ya Kawaida

***92.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara imetengewa bajeti ya Shilingi Bilioni Kumi na Saba, Milioni Mia Tatu Ishirini na Sita, Mia Moja Sabini na Sita Elfu **(Sh.17,326,176,000)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (Matumizi Mengineyo

na Mishahara). Fedha hizo zinajumuisha Mishahara ya Watumishi wa Wizara Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Sita na Tano, Mia Nne Sabini na Saba Elfu **(Sh.3,605,477,000),** Mishahara ya Asasi Shilingi Bilioni Tisa, Milioni Mia Nane Thelathini na Moja, Mia Saba Tisini na Tatu Elfu **(Sh.9,831,793,000),** Matumizi Mengineyo ya Wizara Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Tatu Themanini, Mia Tatu Ishirini na Tatu Elfu **(Sh.3,380,323,000)** na Matumizi Mengineyo ya Asasi Shilingi Milioni Mia Tano na Nane, Mia Tano Themanini na Tatu Elfu **(Sh.508,583,000).** Mchanganuo wa makadirio ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara na Asasi upo katika ***Kiambatisho Na. II.*** Matumizi ya Kawaida kwa Wizara peke yake rejea ***Kiambatisho Na. III*** na kwa Asasi rejea ***Kiambatisho Na. IV.***

**Miradi ya Maendeleo**

***93.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara imetengewa jumla ya Shilingi Bilioni Tatu **(Sh.3,000,000,000)** kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Mchanganuo upo katika **Kiambatisho Na. V**.

## F. MAOMBI YA FEDHA KWA AJILI YA KUTEKELEZA MPANGO WA MWAKA 2016/2017

***94.*** ***Mheshimiwa Spika,*** ili Wizara iweze kutekeleza majukumu na malengo yake ya mwaka wa fedha 2016/2017, naomba sasa Bunge lako Tukufu liidhinishe bajeti ya

jumla ya Shilingi Bilioni Ishirini, Milioni Mia Tatu Ishirini na Sita, Mia Moja Sabini na Sita Elfu **(Sh.20,326,176,000)** ambapo kati ya hizo, fedha za Matumizi ya Kawaida ni Shilingi Bilioni Kumi na Saba, Milioni Mia Tatu Ishirini na Sita, Mia Moja Sabini na Sita Elfu **(Sh.17,326,176,000)** zinazojumuisha Mishahara Shilingi Bilioni Kumi na Tatu, Milioni Mia Nne Thelathini na Saba, Mia Mbili Sabani Elfu **(Sh.13,437,270,000)** na Matumizi Mengineyo Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Nane Themanini na Nane, Mia Tisa na Sita Elfu **(Sh.3,888,906,000)**. Miradi ya Maendeleo ni Shilingi Bilioni Tatu **(Sh.3,000,000,000)**. Mchanganuo wa fedha hizo upo katika viambatisho vilivyotajwa hapo awali ambavyo ni sehemu ya Hotuba hii.

## G. SHUKRANI

***95.*** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kuwashukuru washirika wetu wa maendeleo ambao wametuunga mkono na kutuwezesha kwa hali na mali kutekeleza majukumu ya Wizara yetu. Shukrani hizi ziwaendee wahisani waliotusaidia nikitarajia kuwa wataendelea na moyo huo. Siyo rahisi kuwataja wote lakini nitaje wachache ambao ni Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, Finland, Uingereza, Denmark, Japan, Sweden, Norway, Iran, Cuba, Korea ya Kusini, India, Misri, Uholanzi, Australia, Marekani na Ujerumani pamoja na Mashirika ya Kimataifa

ya United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization (UNESCO), United Nations Development Programme (UNDP), Japan International Cooperation Agency (JICA), International Labour Organization (ILO), na British Council. Wengine ni Umoja wa Ulaya (European Union) na Wafadhili wote wa ndani ambao tumeshirikiana nao katika kutekeleza majukumu yetu katika mwaka 2015/2016, wakiwa ni pamoja na Startimes, National Microfinance Bank (NMB), Tanzania Breweries Limited (TBL), Serengeti Breweries Limited (SBL), AIRTEL, Tigo, Vodacom, Zantel, CRDB Bank na wengine.

***96.*** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuwashukuru Wadau wa Wizara yangu wakiwemo Waandishi wa Habari, Wanamichezo na Wasanii kwa mchango wao uliowezesha Wizara kutekeleza majukumu yake. Aidha, ninaishukuru sana Wizara ya Elimu, Press "A" kwa kuchapa hotuba hii kwa wakati.

***97.*** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda nitoe tena shukrani zangu za dhati kwako binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara kwa anuani ya: www.habari.go.tz, www.wananchi.go.tz na www.tanzaniangovernment.blogspot.com.

***98.*** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

**H. VIAMBATISHO**

*Kiambatisho Na. I*

**MAKUSANYO YA MAPATO KWA MWAKA 2015/2016 NA MAKADIRIO YA MWAKA 2016/2017**

**Idara ya Utawala na Rasilimali Watu**

| Na | Namba ya Chanzo cha Mapato | Chanzo cha Mpato | Makisio ya Mapato 2015/2016 | Makusanyo Julai 2015 hadi Machi, 2016 | Makadirio ya 2016/2017 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | 140283 | Mauzo ya Zabuni | 1,000 | - | - |
| 2. | 140368 | Mapato kutoka vyanzo mbalimbali | 1,000 | - | - |
| 3. | 140370 | Marejesho ya fedha za Umma | 1,000 | - | - |
| **JUMLA NDOGO** | | | **3,000** | **-** | **-** |
| **Idara ya Utamaduni** | | | | | |

| Na | Namba ya Chanzo cha Mapato | Chanzo cha Mpato | Makisio ya Mapato 2015/2016 | Makusanyo Julai 2015 hadi Machi, 2016 | Makadirio ya 2016/2017 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | 140312 | Ukaguzi wa filamu | 65,000,000 | 44,890,345 | |
| 2. | 140370 | Marejesho ya fedha za Umma | - | - | - |
| 3. | 140368 | Mapato kutoka vyanzo mbalimbali | - | - | - |
| 4. | 140386 | Vibali vya kutengeneza filamu | 450,000,000 | 412,202,606 | - |
| **JUMLA NDOGO** | | | **515,000,000** | **457,092,951** | **-** |
| | | | **Idara ya Michezo** | | |

| Na | Namba ya Chanzo cha Mapato | Chanzo cha Mpato | Makisio ya Mapato 2015/2016 | Makusanyo Julai 2015 hadi Machi, 2016 | Makadirio ya 2016/2017 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | 140259 | Mapato ya viwanja vya Michezo (Uhuru na Taifa) | 640,000,000 | 224,650,808 | 640,000,000 |
| 2. | 140315 | Ada za Mafunzo | 40,000,000 | - | 40,000,000 |
| 3. | 140370 | Mapato kutoka vyanzo mbalimbali | 1,000 | - | 1,000 |
| 4 | 140370 | Marejesho ya fedha za Umma | 1,000 | - | 1,000 |
| **JUMLA NDOGO** | | | **680,002,000** | **224,650,808** | **680,002,000** |
| **Idara ya Habari** | | | | | |

| Na | Namba ya Chanzo cha Mapato | Chanzo cha Mpato | Makisio ya Mapato 2015/2016 | Makusanyo Julai 2015 hadi Machi, 2016 | Makadirio ya 2016/2017 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | 140202 | Machapisho ya picha, mabango na majarida | 50,000,000 | 320,512,000 | 50,000,000 |
| 2. | 140264 | Usajili wa magazeti | 30,000,000 | 10,250,000 | 30,000,000 |
| 4. | 140265 | Ukumbi wa mikutano | 30,000,000 | 9,480,000 | 30,000,000 |
| 5. | 140310 | Ada ya mwaka ya Magazeti | 1,000 | - | 1,000 |
| 6. | 140368 | Mapato kutoka vyanzo mbalimbali | 1,000 | - | 1,000 |
| 7. | 140370 | Marejesho ya fedha za Umma | 1,000 | - | 1,000 |

| Na | Namba ya Chanzo cha Mapato | Chanzo cha Mpato | Makisio ya Mapato 2015/2016 | Makusanyo Julai 2015 hadi Machi, 2016 | Makadirio ya 2016/2017 |
|---|---|---|---|---|---|
| 8. | 140387 | Vitambulisho vya Waandishi wa Habari | 25,000,000 | 45,618,650 | 30,000,000 |
| **JUMLA NDOGO** | | | **135,003,000** | **385,860,650** | **140,003,000** |
| **JUMLA KUU** | | | **1,330,008,000** | **1,067,604,409** | **820,005,000** |

**Chanzo:** Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo – Kitengo cha Fedha na Uhasibu

***Kiambatisho Na. II***

**MCHANGANUO WA BAJETI YA MATUMIZI YA KAWAIDA KWA MWAKA**

## 2016/2017 WIZARA NA ASASI

| **IDARA/KITENGO** | **MAKISIO 2016/2017** | | |
|---|---|---|---|
| | **MISHAHARA (PE)** | **MATUMIZI MENGINEYO (OC)** | **JUMLA MATUMIZI YA KAWAIDA (2+3)** |
| **(1)** | **(2)** | **(3)** | **(4)** |
| **1001** - UTAWALA NA RASILIMALI WATU | 1,159,464,000 | 2,691,633,000 | 3,851,097,000 |
| **1002** – FEDHA NA UHASIBU | 246,720,000 | 13,080,000 | 259,800,000 |
| **1003** – SERA NA MIPANGO | 183,780,000 | 83,520,000 | 267,300,000 |
| **1004 –** MAWASILIANO SERIKALINI | 45,480,000 | 18,250,000 | 63,730,000 |
| **1005** - UNUNUZI NA UGAVI | 112,596,000 | 100,000,000 | 212,596,000 |
| **1006** - UKAGUZI WA NDANI | 80,124,000 | 13,080,000 | 93,204,000 |
| **1007 -** TEHAMA | 91,620,000 | 145,000,000 | 236,620,000 |
| **1008 -** SHERIA | 30,960,000 | 30,000,000 | 60,960,000 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **6001** – MAENDELEO YA UTAMADUNI | 2,897,448,000 | 336,391,000 | 3,233,839,000 |
| **0000** – MAENDELEO YA SANAA | - | - | - |
| **6004 –** MAENDELEO YA MICHEZO | 1,023,786,000 | 392,552,000 | 1,416,338,000 |
| **7003 –** HABARI | 7,565,292,000 | 65,400,000 | 7,630,692,000 |
| **JUMLA KUU** | **13,437,270,000** | **3,888,906,000** | **17,326,176,000** |

**Chanzo:** Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo

***Kiambatisho Na. III***

**MCHANGANUO WA BAJETI YA MATUMIZI YA KAWAIDA KWA MWAKA 2016/2017–WIZARA**

| IDARA/KITENGO | MAKISIO 2016/2017 | | |
|---|---|---|---|
| | MISHAHARA (PE) | MATUMIZI MENGINEYO (OC) | JUMLA MATUMIZI YA KAWAIDA (2+3) |
| (1) | (2) | (3) | (4) |
| **1001** - UTAWALA NA RASILIMALI WATU | 1,159,464,000 | 2,691,633,000 | 3,851,097,000 |
| **1002** – FEDHA NA UHASIBU | 246,720,000 | 13,080,000 | 259,800,000 |
| **1003** – SERA NA MIPANGO | 183,780,000 | 83,520,000 | 267,300,000 |
| **1004** - MAWASILIANO SERIKALINI | 45,480,000 | 18,250,000 | 63,730,000 |
| **1005** - UNUNUZI NA UGAVI | 112,596,000 | 100,000,000 | 212,596,000 |
| **1006** - UKAGUZI WA NDANI | 80,124,000 | 13,080,000 | 93,204,000 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **1007 -** TEHAMA | 91,620,000 | 145,000,000 | 236,620,000 |
| **1008 -** SHERIA | 30,960,000 | 30,000,000 | 60,960,000 |
| **6001** – MAENDELEO YA UTAMADUNI | 399,456,000 | 104,640,000 | 504,096,000 |
| **0000** - MAENDELEO YA SANAA | - | - | - |
| **6004** – MAENDELEO YA MICHEZO | 625,488,000 | 115,720,000 | 741,208,000 |
| **7003 –** HABARI | 629,789,000 | 65,400,000 | 695,189,000 |
| **JUMLA** | **3,605,477,000** | **3,380,323,000** | **6,985,800,000** |

**Chanzo:** Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo

***Kiambatisho Na. IV***

**MCHANGANUO WA BAJETI YA MATUMIZI YA KAWAIDA KWA MWAKA 2016/2017 – ASASI**

| TAASISI/MASHIRIKA | MAKISIO YA 2016/2017 | | |
|---|---|---|---|
| | MISHAHARA (PE) | MATUMIZI MENGINEYO (OC) | JUMLA MATUMIZI YA KAWAIDA (2+3) |
| (1) | (2) | (3) | (4) |
| **6001 - 280514**<br>BODI YA FILAMU. | - | 90,162,000 | 90,162,000 |
| **6001 - 280515**<br>BARAZA LA SANAA LA TAIFA (BASATA) | 620,532,000 | 45,081,000 | 665,613,000 |
| **6001 - 280516**<br>BARAZA LA KISWAHILI LA TAIFA (BAKITA) | 699,780,000 | 45,081,000 | 744,861,000 |
| **6001 - 280328**<br>TaSUBa | 1,177,680,000 | 51,427,000 | 1,229,107,000 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **6004 – 280518**<br>BARAZA LA MICHEZO LA TAIFA (BMT) | 398,298,000 | 51,427,000 | 449,725,000 |
| **6004 – 270380**<br>CHUO CHA MAENDELEO YA MICHEZO-MALYA | - | 135,243,000 | 135,243,000 |
| **6004 – 270839**<br>KITUO CHA MICHEZO – ARUSHA | - | 45,081,000 | 45,081,000 |
| **6004 – 270840**<br>KITUO CHA MICHEZO-SONGEA | - | 45,081,000 | 45,081,000 |
| **7003 – 280577**<br>SHIRIKA LA UTANGAZAJI TANZANIA (TBC) | 6,935,503,000 | - | 6,935,503,000 |
| **JUMLA** | **9,831,793,000** | **508,583,000** | **10,340,376,000** |

**Chanzo:** Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo

*Kiambatisho Na. V*

## BAJETI YA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2016/2017

| **PROGRAMU/MRADI** | **MAKADIRIO YA 2016/2017** | | |
|---|---|---|---|
| | **FEDHA ZA NDANI** | **FEDHA ZA NJE** | **JUMLA** |
| **6001 – IDARA YA MAENDELEO YA UTAMADUNI** | | | |
| **6293-**Programu ya Ukombozi wa Bara la Afrika | 700,000,000 | - | 700,000,000 |
| **6355-**Ujenzi wa Ukumbi wa Wazi wa Maonyesho ya Sanaa (BASATA) | 800,000,000 | - | 800,000,000 |
| **4353** Ukarabati wa Chuo cha Sanaa Bagamoyo | 300,000,000 | - | 300,000,000 |
| **Jumla** | **1,800,000,000** | **-** | **1,800,000,000** |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **6004 – IDARA YA MAENDELEO YA MICHEZO** | | | |
| **6523 –** Eneo Changamani la Michezo | 100,000,000 | | 100,000,000 |
| **Jumla** | **100,000,000** | | **100,000,000** |
| **7003 – IDARA YA HABARI** | | | |
| **6567-** Habari kwa Umma | 100,000,000 | - | 100,000,000 |
| **4279-**Upanuzi wa Usikivu-TBC | 1,000,000,000 | | 1,000,000,000 |
| **Jumla** | **1,100,000,000** | **-** | **1,100,000,000** |
| **JUMLA KUU** | **3,000,000,000** | **-** | **3,000,000,000** |

**Chanzo:** Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo